# MKEWE AMEJIWEKA TAYARI

*Ufunuo 19:7 ''Na tufurahi, tukashangilie tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya mwanakondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari.*

Na tumsikilize mjumbe wa Mungu wa wakati wa mwisho:

Yesu alisema, ''kama ilivyokuwa siku za Sodoma ''

Sasa angalia kwa karibu, ''katika siku za Sodoma, hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja kwake Mwana wa Adamu, siku za kufunuliwa kwake Mwana wa Adamu''(Luka 17:28-30).Siyo tena kama kanisa, sio tena Bibi arusi ameshaitwa. ''Siku za Mwana wa Adamu atakapo funuliwa''. Nini? Kuliunganisha kanisa pamoja na kichwa viungane Arusi ya Mwana Kondoo.

Ule mwito wa Bwana Arusi utakuja kupitia hili, wakati Mwana wa Adamu atakaposhuka chini na kuja katika mwili wa kibinadamu kuungana pamoja. Kanisa linapaswa liwe Neno;Yeye ni Neno, na hawa wawili wanaungana pamoja, na ili kufanya hilo itachukuwa udhihirisho wa Ufunuo wa Mwana wa Adamu. Siyo wakuu wa kanisa. Sijui unaona ninachomaanisha?

Unaona, ni Mwana wa Adamu, Yesu Kristo, atakuja chini katika umbile la kibinadamu miongoni mwetu, na kulifanya Neno lake halisi sana kiasi kwamba italiunganisha kanisa na Yeye wawe mmoja, Bibi Arusi, na baadaye ataondoka kwenda nyumbani kwenye karamu ya Arusi. Amina. tayari ameunganika; tunaenda kwenye karamu ya Arusi, siyo kwenye ndoa (Arusi). ''Na tufurahi tukashangilie na kumpa utukufu, kwa maana Arusi ya Mwana Kondoo imekuja''. Unyakuo ni kwenda kwenye karamu ya Arusi. Neno hapa linapoungana na mtu, na hawa wawili wanakuwa mmoja, na hapo sasa linafanya nini? Lina mdhihirisha tena Mwana wa Adamu. Neno na kanisa vinakuwa kitu kimoja. Chochote alichokifanya Mwana wa Adamu, Yeye ni Neno, Kanisa linafanya jambo lile lile.

Mkristo anapookolewa, kwanza, imani yake inaelekezwa kwa Kristo, ndipo ana jambo fulani apaswalo kulifanya mwenyewe. Lazima afanye hivyo, baadaye, kujitakasa kutoka kwa vyote ambavyo ni vichafu, '' kuweka kando kila mzigo,akijifanya tayari (Waebrani 12:1-2).Bibi Arusi amejiweka tayari.''

Kama ukiangalia, alisema, ''amejiweka tayari'', wengi wanasema, kama Bwana ataondoa Roho hii ovu toka kwangu, ulevi, au kamari au uongo, au wizi, nitamtumikia.Lakini hilo ni juu yako. Unapaswa ufanye jambo fulani pia. ''wale washindao watayarithi haya'' wale washindao (Ufunuo3:21,21:7) unao uwezo wa kufanya hivyo (Luka, Mt. 1:12-14), Lakini lazima uwe tayari kuviacha unaona? Amejiweka tayari. Nalipenda hilo Neno.

Sasa, katika mlango-moyo na nafsi yako kuna mmoja tu, lango moja, nalo linaitwa''utashi'' Wewe ni mmiliki wa kitu gani kipite pale. Na inafanya nini? Hii ni nini? Mwili mzima uoshwe,(Waefeso 5:26-27); utakaswe, na hapa ujazwe na Roho Mtakatifu, na hapa panakuwa kiti cha hukumu cha Mungu tena.Ambacho Mungu anakaa moyoni mwako, ufanyapo jambo lisilo sahihi,unasema oh jamani, "nimefanya jambo siyo sahihi''.

Watu wengine wanasema "hainihukumu kuwa na nywele fupi wanawake. Haini hukumu kupaka marangi na mitindo au chochote kile hainihukumu kwenda kwenye dansi, hainihukumu kusema uongo kidogo mweupe,hainihukumu kucheza karata kwenye karamu zetu za karata''. Unajua ni kwa nini? Hakuna kitu cha kuhukumu''.Hiyo haiumizi dhamiri yangu'' kwa kuwa huna dhamiri kama vile nyoka asivyo na nyonga.Huna dhamiri; hakuna chochote kitakacho kuumiza. Wewe ni wa dunia.

Lakini ninakuhimiza umruhusu Yesu Kristo aje (moyoni) hapa na ujaribu kulitenda hilo tena. Ndugu, utahukumiwa sana na kurudi nyuma kuliacha hilo ukitingisha kichwa kuliacha jambo hilo kwa hakika kama vile ilivyo kweli kwamba ninasimama hapa. Kwa sababu yeye ni Mtakatifu.Sikia ninanukuu maandiko, “kama unapenda mambo ya (hiyo dunia) mambo ya dunia, ni kwasababu upendo wa Mungu hauko ndani yako(1Yoh 2:15-17).

Ukoje utashi? Kwanini uite utashi? Ndugu Branhamu? Kwa sababu inamuweka mwanaume na mwanamke kama pale nyuma tena ilivyokuwa kwa Adamu na Hawa pale bustani ya Edeni, kwenye nini? Miti ile miwili? Utashi, mmoja ni wa kifo, mwingine ni wa uzima, utashi……. Uhuru wa kuchagua…….Mungu alimweka mtu wa kwanza, Adamu na Hawa, hapa hapa katika hali ya uhuru wa kuchagua anakuweka wewe mahali pale pale. Na njia pekee ya kulifanya likamilike hapa ni utashi wako.Haleluya utashi wako inabidi upende kufanya mapenzi ya Mungu. Inabidi uondoe mapenzi yako kuruhusu mapenzi ya Mungu kwako, kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee iongozayo kwenye moyo.

Oh, unaweza kujiunga na kanisa, ninyi wabaptisti na wapresbteria. Na ninyi wamethodist na wapilgrim Holiness mnaweza kuja kwenye Utakaso.Lakini inabidi upende kuyafanya mapenzi ya Mungu, utashi, kumruhusu Roho Mtakatifu aje hapa na kuleta; “Ishara hizi zitafuatana nao waamini, kwa jina Langu watatoa pepo,watasema kwa lugha ngeni.Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, au kunywa vitu vya kufisha n.k.(Marko16:17-18) Ishara hizi zitafuatana na hao waliokubali mapenzi yao yawe mapenzi yangu, na kazi ninazozifanya watazifanya’’ naamini halikosi hilo. Kuna kupenda (mapenzi) na kufanya mapenzi ya Mungu. Unaona ninacho maanisha?

Unaona, Mungu asingetusukuma sisi kupita kwenye bomba dogo, na kutuvuta sisi upande mwingine wa mwisho halafu aseme “Amebarikiwa yeye ashindaye” Huna chochote cha kushinda; Yeye amekusukuma ndio ukapita. Lakini unapaswa ufanye maamuzi yako mwenyewe. Yanipasa nifanye maamuzi yangu. Kwa kufanya hivyo tunaonyesha imani yetu na heshima kwa Mungu.

Ibrahimu aliahidiwa mtoto, naye alipaswa aishikilie ahadi hii miaka ishirini na mitano, kule kupanda na kule kushuka ambako alikuwa nako na majaribu katika miaka hiyo ishirini na mitano: Lakini alishikilia Neno la ahadi (Warumi 4:16-22).

Na Israel walipewa ahadi ya nchi ya ahadi. Lakini walipaswa wapiganie kila Inchi yake. Popote pale ambapo nyayo za miguu yenu zitakanyaga, hapo nimewapa ninyi. Mungu alimwambia Joshua (Joshua1:3) Na vyote vilikuwa pale. Ile Nchi ilikuwa pale, na Mungu alikwisha kuwapa wao;bali alipaswa kuipigania Ndivyo ilivyo hivyo hata uponyaji wa kiMungu; Mungu anazo nguvu za kukuponya wewe, kama una ujasiri wa kulipokea, lakini unapaswa kupigania kila Inchi ya hiyo njia. Mungu anayo neema ya kushangaza ya kukuokoa wewe, na atafanya hivyo. Lakini utapigania kila Inchi ya njia yako.

Nabii alisema: Nimekuwa nyuma ya mimbara katika miaka thelathini na moja. Nakila Inchi ya hilo ilikuwa ni vita wakati wote. Ni kweli iko hivyo. Lakini yatupasa tupigane kama tunataka kutawala. Kwa hiyo tunaona kwamba bibi arusi yapasa ajiweke tayari,akubali “kuweka kando kila mzigo unaolemea kwa urahisi, ili tupige mbio kwa saburi ya mashindano yaliyo mbele yetu” Lazima tuweke kando sisi wenyewe. Hatuwezi kusema “Mungu njoo, niwekee kando mzigo huu”. Yatupasa tufanya hivyo wenyewe (Waebrania 12:1-3).

Sasa, angalia, Biblia imesema amejiweka tayari mwishoni mwa wakati.Ni kwa namna gani amejiweka tayari? Ili awe mkewe. Je alifanya……alikuwa na vazi gani amevaa.Neno lake mwenyewe alikuwa amevalishwa katika haki yake (Ufunuo 19:8;1Kor 1:30-31). Hebu natusikie Neno la Nabii juu ya agizo lake vema, watu wote wameniacha, lakini kuna jambo moja, Yeye amesimama nami……. Sikuacha kuyatii yale maono ya mbinguni yaliyo tokea pale chini mtoni.Nimebakia mwaminifu kwa hayo. Naye amekuwa mwaminifu kwangu. Namtumaini Yeye, siku moja sijui ni lini, kwa ajili ya kuivalisha taji huduma yangu. Nitabakia kuwa mwaminifu kwa kadri ninavyoweza kuwa .Sijui itakuwaje, sijui itakuwa lini. Lakini nataka atakapokuwa tayari,mimi niwe. Sasa angalia hapa, Natumaini atavika taji huduma yangu, na hili, ya kuniacha nichukuwe vazi la Neno na kumvika bibi arusi wake katika nguo za Neno na kwa Haki yake. Natumaini atanivika taji na kuniacha nisimame pale siku ile na niseme “Tazama mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu”.

Upinde wa mvua, agano ambalo Mungu amelifanya kupitia Ibrahimu, kupitia Isaka, kupitia Kristo, kupitia kanisa, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Joho la rangi saba lililovaliwa na Josefu, lililokuwa na Yesu; liko pamoja na kanisa leo, likilinda. Ule mwili ulifunikwa na Joho. Na kanisa sio wewe; ni Roho Mtakatifu ambaye amekufanya wewe ufunikwe na damu, Agano la Mungu, iliyo teuliwa kimbele kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu (Efeso 1:3-4) Haleluya.

Mungu ametuosha sisi kwa damu ya mwanae (Ufunuo 1:5-6) na kutusafisha sisi, akatupa vazi la Roho Mtakatifu.Na sasa lile gari kubwa la Mungu litaifungua milango, na tutaenda nyumbani kuishi naye, rekodi zote zitaharibiwa, hatuwezi kuhukumiwa tena; zitachomwa moto, ataziweka kwenye bahari ya usahaulifu na hazitakumbukwa tena (Mika 7:19; Isaya 43:25). Sio ajabu tunaimba, "Neema ya ajabu! Jinsi ilivyo tamu kusikika, ambayo imeniokoa mwovu kama mimi.Nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana, na nilipokuwa kipofu, lakini sasa ninaona".

Hilo ndilo kanisa kama liko kwenye utaratibu (limewekwa kwenye utaratibu), inakuwa……. Mitambo yote iko tayari; inahitaji tu ile nguvu ya kuendesha mitambo.Usiku wa leo tutaweka mitambo yote tayari, weka mioyo yetu kwa usahihi, mambo tuwezayo kufanya, kufuata kila Neno, kumfuata Yeye katika ubatizo wa maji, kumfuata katika utaratibu wote aliotuambia tufanye, mitambo yote iwekwe tayari kusimama pale; sasa hapo tutakuwa tayari kwa zile nguvu za mitambo kuachiwa, na Mungu pekee ndiye awezaye kufanya hivyo; na hilo lidondokee ndani ya moyo wako ile imani ya kusema, "sasa nimeponywa". Hapo haifanyi tofauti kwamba mazingira yakoje, kwa vyovyote umeponywa, kwa sababu ni imani, kwa imani umeponywa.

Wakati huo ambao ameahidi, atakuwepo hapa, na katika siku hizi tutapaa kwenda zetu, iweni tu tayari, yawekeni mavazi ya arusi tayari. Weka ukatiliwote nje ya moyo wako. Na chochote kile………

Naye akaaniambia andika, wamebarikiwa wale walioalikwa karamu ya Arusi ya Mwana Kondoo.akaniambia, maneno haya ni maneno ya kweli ya Mungu (Ufunuo 19:9).

Kwa hiyo kutakuwepo na mkutano hewani katika moja ya siku hizi, katika ule uzuri uzidio. Kaeni tu tayari. Jiwekeni tayari.Takaseni mioyo yenu kutoka mawazo yote maovu. Kuwa na imani na Mungu, haijalishi inaonekana ni giza kiasi gani na vicheko na kudharauliwa kwingi na kule kuambiwa umefanya makosa. Endelea kwa usahihi kuishi maisha Matakatifu kwa Mungu. Endelea kusonga mbele;saa itafika.

Hebu sasa, wakati tunaweza na muda unaturuhusu tujiandae kwa muda huo ujao; kwa maana hatujui utakuwa lini. Hatujui yule atakaye fuatia. Hebu tuishi kwa namna ambayo kama muda utakuja, kwa ajili yetu, tuwe tayari.

Na tunaomba kwa kiasi tunajaribu kumfanya aonekane na watu kwa njia ya Neno. Naye Roho Mtakatifu alihuishe Neno kwa ajili yetu, kwamba tutaweza kujiandaa wenyewe kwa kule kuja kwake.Angalia, huu ni wakati wa kutengeneza na kuwasha taa wakati wa kutoka na kuingia. "Bali wao wamngojao Bwana watapata nguvu mpya" (Isaya 40:30-31).

Sasa tunaona ujumbe wetu ulivyo leo-ujumbe tulio nao wa kutoka Babiloni (Ufunuo 18:4) na kuwa huru, na kujazwa na Roho, na kutengeneza taa, na kuangalia juu, kwa kuwa ukombozi wetu umekaribia (Mathayo 25:6-7); Luka 21:28).

Kwa hiyo tunajua tuko wakati wa mwisho tuko hapa. Sijui ni kwa umbali gani; Yeye hataturuhusu tujue hilo kwa sababu kuja kwake ni kama mwizi wakati wa usiku. Lakini, marafiki,kaka zangu, dada, na tuwe tayari bila kujali.Hebu tujiweke katika unyoofu, unaona, kwa sababu dunia itakuwa tu inaendelea. Hawatajua kwamba limetokea, milango ya rehema itakapofungwa,wahubiri watakuwa bado wanahubiri wokovu, wakiwafanya watu watubu, na wakiendelea kama ilivyokuwa kawaida limefanya hivyo katika nyakati nyingine na itafanya hivyo katika wakati huu. Na unyakuo unakuwa wa ghalfa na wa haraka kiasi kwamba dunia haitaona kama imepoteza au kupungukiwa na watu, kwamba wameshaondoka (1Wathesalonike 4:16-17; 1Kor 15 :51-54).Hiyo ni kweli. Hawatajua kitu juu ya hilo. Anakuja na kumnyakuwa mbali.Itakuwa imeshatendeka, hawatalijua hilo. Hivyo iweni kwenye maombi .Nitawaombea niombeeni na mimi. Hatujui saa ipi,lakini, twamwamini itakuwa hivi karibuni. Kaeni mbali na vitu vya kung'ara. Kaeni na Injili. Unaona? Kaeni hapo sasa na muombe.

## Nukuu katika kiingereza:

kuthibitisha Neno lake, Aya236/"Ufunuo sura ya nne, sehemu ya 1'',aya 64/89-91/ Arusi ya Mwana kondoo 62-0121E),Aya 27-30/Ufunuo, sura ya 4, sehemu ya 111 Aya 121/'' Israeli katika Misri'' (Israel na kanisa,sehemu ya 1). Aya 157- 160/ujumbe wa neema (Kitabu cha 13 na 3)Aya 163/Nimesikia sasa ninaona para 81/ Majina ya makufuru

(kitabu 3 na 21) uk 4/kung'ang'ania (62-0502)Aaya 1 kumfanyia Mungu kazi, Aya 156/Milango ndani ya mlango Aya 39/Yeye aliye ndani yenu, Aya25.

---

*Jiwe la kiroho la kujengea na 99 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*

*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe Tanga*
*E-mail: chaelika@live.com*
*Cell.phone 0784704299/ 0718230098*